

**IKUTHA SUB-COUNTY KCSE REVISION MOCK EXAMS
2015**

**102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
FASIHI**

SCHOOLS NET KENYA
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

FASIHI

JULAI/AGOSTI, 2015

MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA PAMOJA WA JIMBO NDOGO LA IKUTHA, 2015

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

FASIHI

MAAGIZO

- a) Jibu maswali **manne** pekee.
- b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
- c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani, **riwaya, tamthilia, hadithi fupi** na **fasihi simulizi**.
- d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
- e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- f) Kila swali lina alama 20.
- g) Karatasi hii ina kurasa **4**
- h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU YA A: USHAIRI**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Vile lelo walalama, kwa yale ulotendewa,
Huyakumbuki ya nyuma, pindi ulipochachawa,
Ulipotenda unyama, uliona ndiyo sawa,
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Ulizusha uhasama, leo wewe wapagawa,
Walia bila kukoma, tungadhani umefiwa,
Sasa huna usalama, huwezi kujiopowa
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Tenda mambo kwa kupima, usiruke huna mbawa,
Una macho kutazama, na akili umepewa,
Matendo hurudi nyuma, atendaye hurudiwa,
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Dunia haishi njama, sijione umepewa,
Ukadhani usalama, binadamu kuwagawa,
Ukahisi ni wanyama, waso hali kama ngawa,
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Unapotenda zahama, siku yako itakuwa,
Ambapo utaungama, useme umechachiwa,
Na uanze kutetema, ulie umeonewa,
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa.

Maswali.

- a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 2)
- b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alama 2)
- c) Eleza muundo wa ubeti wa pili. (alama 4)
- d) Ni kaida zipi za utunzi zilizozingatiwa na mshairi? (alama 2)
- e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya mjazo. (alama 4)
- f) Toa mifano miwili ya idhini ya mshairi. (alama 2)
- g) Kwa nini msemewa hafai kulalamika ? (alama 2)
- h) Eleza maana ya maneno yafuatayo.
- i) Uhasama (alama 1)
- ii) Umepowa (alama 1)

SEHEMU YA B: RIWAYA***Kidagaa Kimemwozea: Ken Walibora***

2. ...unaa...seema mimiiii sipakui?...wataka mimi nipike? Ehee? Ati mimi nalaza damu? Wewe unaiamsha damu?
- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza mbinu zozote tatu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 6)
- c) Jadili ufaafu wa anwani kwa kurejelea mnenaji. (alama 10)
3. Eleza jinsi mbinu ya tabaini inavyojitokeza katika riwaya ya kidagaa kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA***Mstahiki Meya: Timothy Arege.******Jibu swali la 4 au 5***

4. “Hawa ndio watu muhimu katika ulimwengu wa sasa”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Fafanua mchango wa mrejelewa katika kusambaratisha baraza la Cheneo. (alama 4)
- c) Cheneo imekandamizwa kutokana na wakazi wake kutotumia akili. Fafanua kauli hii kwa kurejelea tamthilia nzima. (alama 12)
5. Tamthilia ya Mstahiki Meya ni taswira kamili ya mataifa mengi barani Afrika. Thibitisha kauli hii. (alama 20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI***Ken Walibora na Said A. Mohamed: Damu Nyeusi***

6. “Hapa huingii bila kuninyoshea mkono...”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza sifa nne za mzungumziwa. (alama 4)
- c) Kwa kurejelea muktadha wa hadithi nzima. Thibisha ukweli wa kauli kuwa mkono mtupu haulambwi (alama 12)
7. Kwa kurejelea hadithi ya Mke Wangu eleza mambo yanayochangia kuimarika kwa ndoa. (alama 20)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Nini maana ya maghani ? (alama 2)
- b) Eleza aina za maghani zifuatazo. (alama 10)
- i) Vivugo
- ii) Tondozi
- iii) Sifo
- iv) Tendi
- v) Rara
- c) Eleza sifa nne za maghani. (alama 4)
- d) Taja umuhimu wa maghani. (alama 4)